**LEARNING BY EAR - "Girls' Rights"**

**EPISODE 7:**

**Title: Peer Pressure – A Story of Girls' Rights**

**AUTHOR: Njoki Muhoho**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Katrin Ogunsade**

**Proof reading: Michael Lawton**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

**Characters:**

Narrator - 30s Male
**SCENE 1 -THE LOCAL TOWN**
Ciro - 14 Female
Cheptoo - 15 Female
Fatuma - 14 Female

**SCENE 2 - PLAYING FIELDS**
Abdi - 15Male
Cheptoo - 15 Female

**SCENE 3 - CIRO PARENT'S HOME**
Ciro 14 Female
Mama Ciro - 40s Female

**SCENE 4 - SCHOOL ASSEMBLY**
Narrator - 30s Male
Fatuma - 14 Female
Headmaster - 40s Male
Group of Students (boys and girls) (14-16)

**SCENE 5 - HEADMASTER'S OFFICE**
Fatuma - 14 Female
Ciro 14 Female
Cheptoo - 15 Female
Abdi - 15 Male
Headmaster - 40s Male

**SCENE 6 - VILLAGE FOOT PATH**

Narrator - 30s Male
Fatuma - 14 Female
Ciro 14 Female
Cheptoo - 15 Female

**SCENE 7 - GIRLS' PARLIAMENT**
Narrator - 30s Male
Fatuma - 14 Female
Ciro 14 Female
Cheptoo - 15 Female
Abdi - 15 Male
Teacher Mona - 35 Female
Janet-Social Worker- 30s Female
Group of Students (boys and girls), 14-16

01. **INTRO**

02. **MUSIC: THEME MUSIC**

03. **NARRATOR** Hujambo na karibu kwa makala ya saba ya 'Learning By Ear' Noa Bongo Jenga Maisha yako katika mchezo kuhusu **Haki za Wasichana**.Katika Kipindi kilichotangulia kwenye mchezo huu tulijadili suala la mizozo ya Kinyumbani na adhabu ya viboko kwa wanafunzi. Na hivi leo tutupia jicho vishawishi vya kuiga tabia na athari zake miongoni mwa vijana. Tuungane na bunge la wasichana wanapojadilia hoja hii.'.

**SCENE 1: THE LOCAL TOWN**

04. **SFX: CITY SOUNDS. CARS HOOT. MUSIC**

05. **FATUMA** (EXCITED) Cheptoo, asante sana kwa kutuleta mjini. Shangazi yako ni mkarimu sana. Natamani tungeweza kukaa kwa muda zaidi.

| | | |
|---|---|---|
| 06. | **CHEPTOO** | Fatuma, Huu ndio urafiki wa dhati. Nashukuru kwamba nina jamaa zangu mjini na kwamba naweza kuja kukaa nao mwishoni mwa wiki na hata wakati shule zinapofungwa. Na Kama marafiki wangu nilionea vyema tuandamane kuja mjini safari hii (PAUSE) Ciro,unaangalia nini ? |
| 07. | **CIRO** | Natazama vipuli vyako na pete. Yaani viko kila mahali, kwenye masikio, puani, ..…na hicho pia ni kipuli kwenye ulimi wako? … yeeeeksss. |
| 08. | **CHEPTOO** | Mmmmmm,,,,! usiwe mshamba hivyo. Huu ndio mtindo wa kisasa . Tazama kila pembe utakuta vijana wengine wakivalia mtindo huu wa kisasa. |
| 09. | **FATUMA** | Lakini.. lakini,.. si lazima ufanye kwasababu vijana wengine mjini wanafanya hivyo |
| 10. | **CHEPTOO** | Fatuma, Fatuma, hebu mtoe ushamba huyu msichana. Tazama sketi yake… unafananana na watu wa kanre iliyopita. |
| 11. | **CIRO** | Cheptoo Sketi yako ni fupi sana, |

| | | |
|---|---|---|
| 12. | **CHEPTOO** | Ni Mini … |
| 13. | **CIRO** | Ndio…hata akili yako pia ni ndogo kama hii Mini. |
| 14. | **CHEPTOO** | (EXCITED) Fatuma, subiri nikutengeneze sketi yako… |
| 15. | **CIRO** | (ALARMED) Cheptoo.. Unafanya nini !! |

**16. <u>SFX: A LOUD RIPPING SOUND</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 17. | **CHEPTOO** | (LAUGHING).Sawa Fatuma, sasa sketi yako imekaa vizuri, fupi lakini bila mkunjo wa chini.! |
| 18. | **FATUMA** | (screaming in protest): Ohhhh Cheptoo umefumua sketi yangu!!! |

**<u>SCENE 2 PLAYING FIEIDS</u>**

**19. <u>SFX: PLAYFIELD NOISES</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 20. | **ABDI** | Cheptoo… Cheptooo, njoo hapa |
| 21. | **CHEPTOO** | Abdi, unafanya nini na rafiki zako hapa? |
| 22. | **ABDI** | (ALARMED) Ongea kwa sauti ya chini Cheptoo. Shika.. piga moshi mmoja |
| 23. | **CHEPTOO** | Ni nini hii? |

| | | |
|---|---|---|
| 24. | **ABDI** | Ni sigara….. Sigara maalum. (GIGGLES) |
| 25. | **CHEPTOO** | Mtashikwa nyinyi… |
| 26. | **ABDI** | Hii! …Hii ndio hunifanya nijisikie niko sawa kabisa. Piga pafu kidogo. Ama bado wewe ni Mtoto ….. Kwak…kwak… |
| 27. | **CHEPTOO** | (SHOUTING) Wacha… wacha hebu nipe hiyo sigara. |

**<u>SCENE 3: CIRO PARENTS' HOME</u>**

**28. <u>SFX: NIGHT SOUNDS</u>**

**29. <u>SFX: WINDOW OPENS SLOWLY. A CRASH</u>.**

| | | |
|---|---|---|
| 30. | **MAMA CIRO** | Nani…? Ni nani huyo? |

**31. <u>SFX: QUICK STEPS</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 32. | **MAMA CIRO** | (SHOCKED) Ciro. … Unafanya nini sakafuni? Kwanini umejifunika mwili mzima? Kwani umefika sasa hivi….? Na umepitia wapi.. dirishani? |
| 33. | **CIRO** | Samahani….. Samahani Mama , nimeanguka |

34. **MAMA CIRO** (VERY ANGRY) Usinidanganye. Umetoroka hapa nyumbani ukaenda wapi. Umekuwa wapi?

35. **CIRO** Eeeh.. nilikuwa… nilikuwa

36. **MAMA CIRO** (SHOUTING).Umekuwa wapi? Niambie haraka la sivyo nitamweleza Babako

37. **CIRO** Samahani Mama, Rafiki yangu Cheptoo na Abdi jana usiku walinipeleka kwenye Disco mjini.

38. **MAMA CIRO** Sasa umejitia mshakani msichana wewe. Tulale tutayazungumze kesho asubuhi.

**39. <u>SCENE 4 SCHOOL ASSEMBLY</u>**

40. **<u>Narrator:</u>** Asubuhi mwalimu mkuu wa shule aliwaita wanfunzi wote katika ukumbi wa shule hiyo. Sikiliza aliyokuwa nayo ya kuzungumza.

**41. <u>SFX: STUDENTS MURMURING</u>**

42. **HEADMASTER** (ANGRY) Kimya kila mmoja.. KIMYA! Nimesikitishwa sana na tabia ya baadhi yenu hapa. Wengi wenu wameanza kuwa na utovu wa nidhamu. Na muliyofanya kamwe hayawezi kukubalika katika shule hii. Mlikutikana katika pembe moja ya shule hii mkinywa pombe na kuvuta sigara

**43. <u>SFX; STUDENTS GASP</u>**

44. **HEADMASTER** Sio tu mlijihusisha na vitendo vya kunywa pombe visivyokubalika kwa watoto walio chini ya miaka 18, bali pia ni makosa kuleta pombe na sigara shuleni na kuwashawishi wengine kunywa na kuvuta sigara.

Nataka kuwaona wafuatao ofisini mwangu mara moja baada ya mkutano huu.; Abdi Kamau, Tunis Kabra, Cheptoo Joseph, Fatuma Jacobs, Ciro Fabio.

FADES OFF

| | | |
|---|---|---|
| 45. | **FATUMA** | (LOUD WHISPER) Oooh Babangu Mzee Jacob ataninichinja! |
| 46. | **NARRATOR** | Nuksi sasa imeingioa shuleni. Endelea kusikiliza ufahamu kitakachotokea katika ofisi ya Mwalimu mkuu.. |

**SCENE 5 HEADMASTER'S OFFICE**

**47. SFX: Knocking on door, Door opens, students come in**

| | | |
|---|---|---|
| 48. | **HEADMASTER** | (ANGRY) Fanyeni haraka, mmeiletea aibu shule hii. Nataka kujua chanzo cha mambo haya kabla sijamfukuzwa kwenda kuwaleta wazazi wenu.Nani alileta Pombe?<br>(FURIOUS) Nasubiri jibu!! |
| 49. | **CHEPTOO** | Ni Abdi na rafiki zake |
| 50. | **ABDI** | Si mimi mwalimu Mkuu ni James |
| 51. | **CIRO** | Mimi sikunywa Mwalimu, Nilionja tu wakati Cheptoo alinilazimisha, na mimi sikutaka. Nilikuwa nikiwatazama wakinywa.. |
| 52. | **HEADMASTER** | Na wewe Fatuma? Mbona kimya. |

53. **FATUMA**

Cheptoo aliniambia kwamba ni mshamba na nilihitaji kuchangamshwa. Kama unavyofahamu ni rafiki yangu mkubwa. Alinisaidia sana wakati wazazi wangu walitaka kuu…

54. **HEADMASTER**

Nyamaza.. kimya kila mmoja. Mnafahamu mlichokuwa mkufanya.Mlijaribu kuwashawishi wengine kujiingiza katika tabia mbovu. Na tabia hii sharti ikome mara moja. Na hivyo nimemfukuza shuleni kwa muda wa wiki mbili. Nendeni nyumbani kuwaleta wazazi wenu kesho asubuhi kabla ya kuchukua barua zenu za kuwafukuza shule .Sasa ondosheni sura zenu ofisini mwangu… nje , nje…..

**55. BRIDGE MUSIC**

**SCENE 6 VILLAGE FOOT PATH/outside atmosphere**

56. **FATUMA**

Ciro, Cheptoo, Tufanye nini sasa? Nitawaambia nini wazazi wangu mimi. Unaona mashaka uliyoniletea Cheptoo.

| | | |
|---|---|---|
| 57. | **CHEPTOO** | (ANGRY) .. Eti nini, Matatizo gani niliyokuletea? Kwanini unataka kunilaumu bila sababu Wewe mwenyewe umejiletea balaa yote hii. |
| 58. | **CIRO** | Cheptoo, wacha kuzungumza kwa sauti ya juu. Kama si wewe na hayo mambo yako . sijui mitindo ya kisasa, hatungekuwa tumekutana na wavulana hawa wakinywa. |
| 59. | **CHEPTOO** | Sasa wataka kunilaumu.Wewe unasababu ya kunilaumu kweli wakati ni wewe uliyekuwa ukibugia pombe na kuvuta sigara!. Ulikuwa ukifurahia wakati huo kwa hivyo wacha kunilaumu. |
| 60. | **FATUMA** | Wewe ulitufanya tunywe pombe. Kwanza ulinifanya nijihisi mshamba kama singekunywa pombe. Hebu Ciro mwambie |
| 61. | **CIRO** | Ni kweli Fatuma…unahitaji kushauriwa kila wakati. |
| 62. | **FATUMA** | Pia wewe Ciro… unataka kunilaumu kwa yote yaliyotokea |

| | | |
|---|---|---|
| 63. | **CHEPTOO** | Sisi ni marafiki. Yamemwagika. Tulishaiwshiwa na tukaingia kwenye mtego. Nyamazeni, sasa nafikiri tumepata hoja ya kuiwasilisha kwenye bunge letu la wasichana. Kwanini tusiwaite wanafunzi wote waliofukuzwa na pia kumwalika mwalimu Mona baada ya masomo. |
| 64. | **CIRO** | Wazo zuri, pia tumwalike Janet afisa wa masuala ya Jamii.! |
| 65. | **FATUMA** | Kwani mmesahau kwamba tumefukuzwa shuleni.. |
| 66. | **CHEPTOO** | Nisikilizeni, nina wazo. Twendeni nyumbani tukawaeleze wazazi kwamba tumefukuzwa kwa muda wa wiki mbili na kwamba wanahitajika wafike shuleni kesho asubuhi, lakini pia tuwafahamishe kuhusu wazo letu. Kwamba tulijadiliane katika bunge letu la wasichana jinsi vishawishi vya kuiga tabia vinavyowathiri vijana. |
| 67. | **CIRO** | (INTERRUPTS) Pia tunaweza kuwaalika pamoja na mwalimu wetu mkuu kuja kusikiliza mjadala huo. |

68. **FATUMA** Hilo ni wazo zuri sana. Pia lazima tuwaalike Mwalimu Mona na Janet, afisa wa masuala ya jamii kwani wamekuwa msingi wa ushauri bora katika bunge letu..Mbali na hayo wanauzoefu wa kupunguza harisa zinapopanda miongoni mwa washiriki.!

69. **CHEPTOO** Tukiweza kuwasadia wasichana wengine wasitumbukie katika vishawishi hivi, pengine Mwalimu mkuu anaweza kutusamehe.

70. **CIRO/FATUMA** Saaaaawa kabisa twendeni..

71. **CHEPTOO** Lakini Mwalimu mkuu akikataa, basi tutaendelea kutekeleza adhabu hiyo. Isitoshe tumepatikana na hatia.

72. **CIRO/FATUMA** (LOUD SIGH) Oooh!

73. **NARRATOR** Je Shule itawakubalia wasichana hawa watatu kuandaa kikao cha mjadala wakati wamefukuzwa shuleni?. Endelea kusikiliza kufahamu zaidi iwapo watafaulu kuandaa kikao hicho.

**SCENE 7 GIRLS' PARLIAMENT**

74. **SFX** **AGGRESSIVE MURMURING**

| | | |
|---|---|---|
| 75. | **CHEPTOO** | Abdi, Ni makosa yako |
| 76. | **ABDI** | Hapana ni makosa yako Cheptoo! Wewe na Ciro! |
| 77. | **TEACHER MONA** | Tosha..Tosha,…Tosha, kimya kila mmoja!! Janet wewe ni afisa wa masuala ya Jamii tuongoze katika mjadala huu kabla ya hawa vijana hawajaanza kupigana |
| 78. | **JANET** | Wavulana na wasichana, huu si wakati kwa kuzozana. Nina hoja ninayotaka kuiwasilisha kwa bunge hili. Mara nyingi nyinyi ndio munaowasiloisha hoja hizi kuhusu masuala yanayowakumba.Hoja yetu leo ni 'Kwanini Vijana wengi hushawishika kujiingiza katika tabia mbovu?' |
| 79. | **FATUMA** | Janet, Vishawishi ni nini? |

| | | |
|---|---|---|
| 80. | **JANET** | Wavulana na wasichana nyinyi ndio chanzo cha visahwishi hivi. Nyinyi ndio huwashawishi vijana wa rika lenu kujiingiza katika mambo mabaya au mazuri.. Kilichotokea hapa ni kwamba baadhi yenu waliwashawishi wengine ili kuonekana kwamba wanakwenda na wakati. |
| 81. | **CHEPTOO** | Kwa hiyo unapendekeza tufanye nini. Tayari tuko mashakani? Tumefukuzwa shuleni. |
| 82. | **TEACHER MONA** | Kwanza kabisa tuchunguze ni kina nani wamo hatarini ya kutumbukia katika vishawishi hivi. Hawa ni vijana ambao hawajiamini maishani na wanajihisi pweke.Vijana ambao hawatangamani na wenzao na wamefadhaika . |
| 83. | **JANET** | Pili lazima uchague marafiki zako kwa uangalifu sana.Marafiki ambao watakukuza kifikra. Wenye maono |

84. **TEACHER MONA** Wakati wote jifunze kukabiliana na vishawishi vya aina hii. Hii inawezekana kwa kujipa moyo na kujiamini wewe mwenyewe. Lazima ujivunie mafanikio yako na sio kuiga wengine wanaotaka kujionyesha maishani..

85. **JANET** Pia lazima uwe na msimamo katika masuala kama vile unywaji wa pombe, madawa ya kulevya, ngono ya mapema na kadhalika.Uwe tayari kuzungumza na wenzako na kwa uwazi kabisa.

86. **CHEPTOO** Huo ni ushauri mzuri sana. Sasa wasichana ni upi msimamo wenu kuhusu pombe na madawa ya kulevya. Labda tunaweza kuanzia hapo.

87. **CIRO** Cheptoo, Kwani umesahau kwamba tumefukuzwa shuleni. Bado adhabu hiyo inatekelezwa

88. **FATUMA** Lakini ni nawazo jingine hapa. Kwanini tusipendekeze kwa mwalimu mkuu kwamba shule nzima ihushishwe katika mjadala huu kwa vikundi?

89. **TEACHER MONA** Pia si wazo baya.

90. **CHEPTOO** Twendeni ofisini kwa Mwalimu mkuu.

**91. THEME MUSIC**

**92. OUTRO**

93. **NARRATOR** Na hadi hapo tunafika mwishi wa makala ya leo ya Noa Bongo jenga maisha yako. Iwapo ungependa kusikiliza tena kipindi hiki au vingine vya Noa bongo, tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine tutakapoungana nawe tena kwa makala nyingine kwaheri kwa sasa.